| | | | |
|---|---|---|---|
| JINA LA MTAHINIWA | | NAMBARI YA MTAHINIWA | |
| JINA LA SHULE YAKO | | NAMBARI YA SHULE | |
| SAHIHI YA MTAHINIWA | | TAREHE | |

004-2025
902/2

# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

JESMA 004

## GREDI YA 9

Karatasi ya 2
Muda: Saa 1 Dakika 45

## - KISWAHILI 902/2-

(*Insha na Utangulizi wa Fasihi*)

- KISWAHILI KARATASI YA 2 -

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. Andika **jina lako** na **nambari yako** ya mtihani kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
2. Andika **jina** na **nambari ya shule yako** kwenye nafasi uliyoachiwa hapo **juu**.
3. Tia sahihi kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
4. Andika **tarehe** ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; **A** na **B**.
6. Jibu maswali **yote.**
7. Andika majibu **yote** kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| **SEHEMU** | **A** | **B** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Zoezi I** Swali:1 | **Zoezi II** Swali: 2 | **Zoezi III** Swali:3 | **Zoezi IV** Swali:4 | **Zoezi V** Swali:5 |
| Alama ya upeo | **15** | **10** | **10** | **10** | **5** |
| Alama ya mtahiniwa | | | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Geuza ukurasa**


Tovuti: www.jesmapublishersltd.com Baruapepe: jesmapublishers@yahoo.com
©*Jesma Publishers & Educational Boosters Ltd. Simu: 0794677748/0701545759*
*WARNING: It is an offence to reproduce, copy or transmit whole or part of this paper on any social media platform. Any person contravening this is liable to criminal prosecution and civil claims for damages.*

CamScanner

## SEHEMU A: (Alama 15)

## ZOEZI I - INSHA.

**Maagizo:**

i) **Inapendekezwa uchukue muda wa dakika 40 katika zoezi hili.**

ii) **Andika insha yenye maneno kati ya 300 - 350 katika nafasi uliyoachiwa.**

*Endeleza mwanzo wa insha hii.*

*Wiki iliyopita, wanafunzi wa Gredi ya Tisa waliamua kuyatunza mazingira katika shule yao. Mwanzo*......................................................................



CamScanner

## SEHEMU B (Alama 35)

## ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

**Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Hapo zamani za kale katika kitongoji cha Mawega, paliishi Fisi na Sungura. Walikuwa marafiki wa kula kusaziana. Walishirikiana kama ngoma na mkwiro katika kazi yao ya ukulima na ufugaji hadi wanyama wengine wakawaonea gere. Mvua nayo iliwakubali , ilinyesha msimu baada ya msimu.

Mashamba yao yakanawiri na maghala yao yakalalamikia shibe. Mifugo wao walikuwa wakupigiwa mfano katika vijiji Jirani kutokana na afya zao za kupendeza. Kadri siku zilivyoyoyoma, ndivyo udugu wao ukaendelea kukita mizizi kweli kweli.

Siku za neema zilipisha za shari. Urafiki wao ukakabiliwa na mtihani mkubwa. Mvua ilikataa kuzuru kijiji chao kwa miaka miwili mtawalia.

Akiba ya chakula walichokuwa wameweka ilianza kupungua na hatimaye chakula kikaadimika mfano wa wali wa daku. Fisi aliuona mustakabali wa maisha ya wana wao ukifunikwa gubigubi na giza totoro. Aliwaza na kuwazua jinsi ya kujikwamua kutoka kwenye shida hii tayari iliyobisha hodi. Hata hivyo hakupata jibu ng'o!

"Bwana wee,njaa inaendelea kutushambulia bila chembe ya huruma. Ukame umefanya mifugo wetu kupungua kwa kiwango kikubwa. Hali ikiendelea hivi, watoto wetu watakuwa kitoweo cha mbweha." Fisi alimwambia Sungura asubuhi moja walipokuwa wakinywa chai ya mkandaa maadamu maziwa yalikuwa muhali kupatikana.

"Ndugu mpendwa, janga hili la njaa ni tokeo la hasira ya mizimu. Mababu wetu walikosa, nasi hatuna budi kutatua laana hii. Jana usiku mizimu ilinijia usingizini. Wala sidhani hata nilikuwa nimelala. Niliiona kwa haya yangu mawili, ikiniambia kwamba njia ya pekee sisi na familia zetu kujiokoa ni kwa kuitolea kafara ili kuituliza. Mizimu yenyewe iliweka nadhiri kuwa tukifanya hivyo, mvua itanyesha mara moja nasi tutazinusuru roho za wana wetu," Sungura alisema na kuyasindikiza maneno yake kwa kilio cha ghafla.

Uso wa Fisi uling'aa kwa furaha ghaya. Hata kabla furaha ile kuyeyuka, alikumbuka jambo. "Ndugu, mifugo wetu wote wamesalimu amri ya ukame. Hata maghala yetu yanaenda miayo kwa kukosa cha kuhifadhi. Hili litawezekana vipi?" Fisi aliuliza

"Ndugu unajua kwamba hata tungekuwa na nafaka, mizimu yenyewe haitaki mbegu, inataka damu, tena si damu yangu wala yako. Inataka damu ya mama zetu. Ndio ambao wamekula chumvi nyingi, hivyo mizimu inawapendelea zaidi," Sungura alisema machozi yakimtiririka tiriri njia nnenne.

Masikio ya Fisi yalivuma kwa uchungu. Moyo ulimsihi alikatae wazo hilo la Sungura; lakini akapiga moyo konde aliamua kulitekeleza wazo hilo. Usiku huo, Fisi alimfikisha mama yake kwenye mbuyu uliokuwa karibu na mto na akamtia kisu kooni huku machozi ya masikitiko yakimpofusha. Mama yake alikata roho huku Fisi akirudi nyumbani akifikiri Sungura amefanya vile walivyoagana.

Fisi aliondoka kwa utulivu moyoni. Usiku huo, mvua kubwa ilianguka na asubuhi ilipofika, mashamba yao yakajaa chakula mara moja. Zizini pia Ng'ombe wakasikika wakikoroma huku ardhi ikitwaa rangi ya kijani kibichi. Wakati huo wote Sungura



CamScanner

hakuonekana nyumbani. Fisi alidhani alikuwa ameenda kujikunyatia kwenye mbuyu kwa huzuni ya kumpoteza mama yake mpendwa. Ghafla bin vuu Fisi alikutana na mama yake Sungura akiwa amebeba mtungi wa maji akielekea nyumbani. Mwili wa Fisi ulikufa ganzi. Malaika yakamsimama na mate kumkauka kinywani.

"Kumbe Sungura hakumtoa kafara mama yake?" Fisi alijisemea huku fundo chungu la chuki na kisasi likimkaba kooni na kukatalia pale kwa sababu hakuamini macho yake.

Huo ndio uliokuwa mwisho wa urafiki kati ya Sungura na Fisi. Tangu siku hiyo , Fisi angali anamtafuta Sungura alipize kisasi.

1. Hii ni hadithi ya aina gani? **(Alama1)**

_______________________________________________

2. Toa sifa mbili zinazotambulisha kuwa hadithi hii ni ya fasihi simulizi. **(Alama 2)**
   a) _______________________________________________
   b) _______________________________________________
3. Taja ujumbe unaojitokeza katika hadithi hii. **(Alama 1)**

_______________________________________________

4. Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika hadithi hii. **(Alama 2)**
   a) _______________________________________________
   b) _______________________________________________
5. Taja njia mbili zinazoonyesha umuhimu wa hadithi katika jamii. **(Alama 2)**
   a) _______________________________________________
   b) _______________________________________________
6. Unajifunza nini kutokana na wahusika wafuatao? **(Alama 2)**
   i) Sungura

_______________________________________________

_______________________________________________

   ii) Fisi

_______________________________________________

_______________________________________________

## ZOEZI III: NOVELA (Alama10)

**Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali.**

Maskini! Kiangalie kilivyotulia hapa! Laiti kingalijua! Nadia aliyarudia maneno haya akilini. Alikuwa amekikodolea macho ya imani kitoto ambacho kilikuwa kimelala pale kivulini. Alikiajabia kijuso cha kitoto hiki.

Chenyewe kilikuwa laini, chenye tabasamu. Lakini alipokichunguza zaidi aliona sikitiko lililokuwa limejificha kwenye ngozi hii ya maji ya kunde. Alikaribia kilipokuwa kitoto na kukishika kwenye kibega cha kulia. Sijui kwa nini alifanya hivyo. Pengine ungemuuliza angekwambia kwamba ilikuwa njia ya kukihakikishia kitoto hiki kwamba kilikuwa salama chini ya ulinzi wake.

Mbele kule alimwona mama yake, Bi. Chanda, ameushika mpini wa jembe lake, au tuseme kiserema chake. Alikuwa anapambana na magugu katika shamba hili ambalo lilikuwa na upana wa bahari.

Nadia alipomtundulia macho kiumbe huyu ambaye alikuwa amempa uhai, hakuweza kujizuia kumwonea Imani. Mgongo wake ulikuwa umejipinda. Usidhani ni kwa uchovu au kupambana na joto la jua la utosini lililokuwa linaiadhibu ngozi yake laini. La! Picha ambayo Nadia alikuwa anatazama ilikuwa matokeo ya dhiki; dhiki ya njaa, dhiki ya fikira za kutwa na kucha kuhusu hali ya maisha ya mumewe na wanawe.

Huenda usielewe hali ya mama huyu, lakini pengine ungekuwa katika hali hiyo hiyo tu. Usiku wa kuamkia Jumatano hii, ni kana kwamba familia ya Bi.Chanda ililala matumbo yakinguruma kama radi. Ukimuuliza Nadia mwenyewe atakwambia kuwa hali ilikuwa 'as above'. Yaani, kama kawaida, walilala vyanda vi kinywani, si kwa majuto bali kwa njaa iliyowauma kama nge. Kidogo walichotia huko hakikufaa chochote.

Kadri Nadia alivyozidi kumtumbulia macho Bi. Chanda, ndivyo kifua chake kilivyozidi kujaa hisia tele, hisia za masikitiko, hisia za kuvunjikiwa, hisia za kutamani hali kuwa bora.

1. Taja aina mbili za mandhari katika kifungu hiki cha novela. **(Alama 2)**

a) ______________________________

b) ______________________________

2. Nandia ni mnyenyekevu kutokana na vile anavyonyenyekea kwa mama yake. Eleza sifa nyingine mbili za Nandia kutokana na kifungu hiki. **(Alama 2)**

a) ______________________________

b) ______________________________

3. Taja na uthibitishe mbinu **tatu** za lugha zinazojitokeza katika sehemu hii ya novela. **(Alama 3)**

a) ______________________________

b) ______________________________

c) ______________________________

4. Taja ujumbe unaojitokeza katika kifungu hiki. **(Alama 2)**

______________________________

______________________________

5. Kamilisha methali hii: **(Alama 1)**

Achanikaye kwenye mpini ______________________________

6. Eleza dhamira ya mwandishi katika sehemu hii ya novela. **(Alama 1)**

______________________________

______________________________

## ZOEZI IV: TAMTHILIA (Alama 10)

**Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali.**

(*Ofisini kwa Afisa wa Elimu,Kaunti ya Ulefo. Mezani kuna faili, gazeti, simu ya mkononi na barua kadha. Anafunuafunua gazeti na kuachana nalo.Mara simu yake inalia.Anaichukua na kuanza kuongea.)*

**Ochipe :** Naam. Ndiye unayeongea naye. Nani mwenzangu? Enhee! Niambie, Bwana Kwaku. Amekutuma kwangu mkuu wa Baraza la Wazee?

Sawa, nakuruhusu kumwakilisha, lakini akirudi kutoka Ndakwet, nitataka kusema naye. Sawa, karibu.*(Anarudisha simu mezani. Mlango inabishwa. Anapaaza sauti na kumkaribisha anayebisha. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Michame anaingia).* Tafadhali keti, Bwana Mwashi.

**Mwashi :** Asante.

**Ochipe :** Habari za Michame?

**Mwashi :** Michame ni ukame tu. Hata wakazi wake **wanapania** kuhama ili kusalimisha mifugo wao.

**Ochipe :** *(Akitikisa kichwa kwa masikitiko.)* Balaa tupu. Uliniambia shule yako ina watoto wangapi?

**Mwashi :** Tisini.

**Ochipe :** Imagine watoto tisini waachishwe shule ili wazazi wao waende nao kutafuta malisho! No, no, no! We must do something.

**Mwashi :** Mimi pia naona hivyo, lakini what can we do?

**Ochipe :** (*Akisukuma faili juu ya meza kuelekea upande wa mgeni wake.)* Hii hapa barua yenyewe, japo walioiandika walificha majina yao.

**Mwashi :** *(Anavuta faili na kuanza kusoma barua kwa hamu. Anatikisa kichwa kwa masikitiko.)* Kweli barua hii inatia huruma.

**Ochipe :** Unaweza kuwatambua walioiandika?

**Mwashi :** (*Anaitupia jicho tena ile barua)* Bila shaka huu ni mwandiko wa Lulu. Ni msichana wa Gredi ya Saba. Inaonekana alishirikiana na mdogo wake kuiandika. Mdogo wake, Slia yuko katika Gredi ya Tano.Wote ni wanafunzi hodari sana.

**Ochipe :** Basi hao ndio mashujaa wa rika lao.

**Mwashi :** Kweli kabisa. Kilio wanachotoa ni kilio cha wote.

**Ochipe :** Ningependa kukutana na waandishi wa barua hii ili niwapongeze kwa ujasiri wao.

**Mwashi :** Hilo linaweza kupangwa baadaye. *(Kunasikika hodi mlangoni.)*

1. Mazungumzo ni mojawapo ya vipera vya tamthilia.Toa mifano mingine miwili ya tamthilia ambayo inajitokeza katika sehemu hii. **(Alama 2)**

   **a)** ____________________

   **b)** ____________________

2. Mwalimu Mkuu anazungumza na nani kwenye simu? **(Alama 1)**

   ____________________

3. Fafanua sifa mbili za waandishi wa barua hii. **(Alama 2)**

   **a)** ____________________

   **b)** ____________________

4. Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika tamthilia hii. **(Alama 2)**

   **a)** ____________________

   **b)** ____________________

5. Eleza umuhimu wa maelezo yaliyo kwenye mabano katika tamthilia hii.**(Alama 1)**

   ____________________


CamScanner

6. Taja mandhari ya onyesho hili. **(Alama 1)**

7. Neno **wanapania** limetumika katika tamthilia hii.Unafikiri lina maana gani? **(Alama 1)**

## <u>ZOEZI V :USHAIRI</u> (Alama 5)

**<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali</u>**

Wito nimeitikia, elimu ni kila kitu,
Wanafunzi karibia, mawazo yasiwe butu,
Shuleni tukiingia, tutoke tukiwa watu,
Masomo kweli bahari, tuogelee kwa ustadi.

Vitabu tukichambua, akili pevu tapata,
Mafumbo tayafumbua, maarifa 'tayakamata,
Kurasa tukifungua, nyayo tutazifuata,
Masomo kweli bahari, tuogelee kwa ustadi.

Walimu wametufunza, kujikaza ni lazima,
Maisha tukiyatunza, tutaukwea mlima,
Umakini uwe kwanza, tutaepuka kukwama,
Masomo kweli bahari, tuogelee kwa ustadi.

Darasani ukifika , zingatia utulivu,
Fahamu unachotaka, uepuke maumivu,
Kila wakati andika, usikubali uvivu,
Masomo kweli bahari, tuogelee kwa ustadi.

Mwakani kunapokucha, gredi nyingine kubisha,
Kumbukizi ziwe picha, tulipotumia shisha,
Kandokando tukificha,mwishowe tashirikisha,
Masomo kweli bahari, tuogelee kwa ustadi.

*(kutoka jungukuu Afrika)*

1. Shairi hili ni la bahari gani? **(Alama 1)**

2. Taja ujumbe mmoja unaojitokeza katika shairi ulilolisoma. **(Alama 1)**

3. Je dhamira ya mwandishi wa shairi hili ni ipi? **(Alama 1)**

4. Taja mbinu moja ya lugha inayojitokeza katika shairi hili. **(Alama 1)**

5. Taja muundo wa shairi hili ukirejelea vina. **(Alama1)**



CamScanner